**MAHAKAMA KUU YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**(MASIJALA NDOGO YA IRINGA)**

**ILIYOPO IRINGA.**

**RUFAA JINAI NA. 9788 YA 2024**

*(Asilia Shauri la Jinai Na. 49/2023 la Mahakama ya Wilaya ya Iringa mbele ya Mhe. S.A. Mkasiwa, HMM).*

**DOTTO KISINGA..............................................................MRUFANI**

**DHIDI YA**

**JAMHURI.................................................................... MRUFANIWA**

**HUKUMU**

*10 & 11 Juni, 2024*

**I.C. MUGETA, J:**

Mrufani anashitakiwa kwa kosa la kujamiiana kwa maharimu kinyume na kifungu cha 158(1)(a) na 161 vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu [Sura ya 16 Toleo Rekebu la 2022]. Hati ya mashtaka inaeleza kuwa mnamo tarehe 15/4/2023, mrufani alimwingilia kingono mtoto wake wa kumzaa wa kike mwenye umri wa miaka 6.

Hakimu Mkazi Mkuu aliyesikiliza shauri hili aliridhika kuwa kosa lilitendwa na mrufani kulingana na ushahidi wa mashahidi wanne walioletwa na upande wa mashtaka. Kwa sababu hiyo alimtia mrufani na kumfunga gerezani kifungo cha maisha kama ilivyo sheria.

Mrufani hakuridhika na vyote, adhabu na hatia hivyo alikata rufaa yenye sababu 9 za rufaa. Lalamiko la msingi katika sababu hizo 9 ni kwamba mashtaka dhidi yake hayakuthibitishwa bila kuacha mashaka ya msingi.

Siku ya kusikiliza rufaa hii mrufani alieleza kwamba hajui kusoma wala kuandika hivyo anaomba maelezo aliyoandaliwa na wenzake gerezani yapokelewe na mahakama iyatumie kama hoja zake kuunga mkono sababu zake za rufani. Winfrida Mpiwa, Msomi Wakili wa Serikali, hakuwa na pingamizi kwa vile Jamhuri nayo inaunga mkono rufaa hii kwani shtaka halikuthibitika. Maelezo hayo ya mrufani yalipokelewa na kupewa alama "doc A" kwa ajili ya rejea. Baada ya hapo mrufani alisema hana cha kuongeza.

Kwenye hoja zake, mrufani ameeleza mambo mengi lakini nitaeleza ninayodhani ni ya msingi pekee.

Hoja ya kwanza ni kwamba hakuna ushahidi kuwa tukio lilitendeka tarehe 15/4/2023 kama inavyodaiwa kwenye hati ya mashtaka. Hoja hii iliungwa mkono na Winfrida Mpiwa, kwa sababu katika ushahidi wake mhanga (SM2) hakueleza tarehe ya tukio. Kwamba tarehe ya tukio imetajwa na mpelelezi (SM3) ambaye ushahidi wake ni wa kuambiwa. Msomi Wakili Winfrida alieleza kuwa pale ambapo tarehe na muda wa tukio vimetajwa katika hati ya mashtaka, lazima vithibitishwe katika ushahidi. Katika kesi hii, alihitimisha, ushahidi huo haupo. Aliirejesha mahakama kwenye shauri la

**Salum Rashid Chitende dhidi ya Jamhuri**, Shauri la Rufaa Jinai Na. 204/2015 Mahakama ya Rufani – Mtwara (haijaripotiwa) kuhusu msimamo huo wa kisheria.

Ninakubaliana na hoja ya mrufani, inayoungwa mkono na upande wa Jamhuri kwamba, tarehe ya tukio iliyotajwa kwenye hati ya mashtaka haikuthibitishwa. Kwa kutothibitisha tarehe ya tukio maana yake hati ya mashtaka haijathibitishwa

Kabla sijaendelea na malalamiko mengine, nitaeleza muhtasari wa ushahidi wa mashtaka ili msingi wa uamuzi wangu ueleweke vizuri.

Mhanga na mrufani ni baba na mtoto wake. Wanaishi nyumba moja pamoja na mama yake mhanga (mke wa mrufani) na watoto wao wengine wawili wa kiume. Mrufani, mkewe na watoto hao wa kiume hawajawahi kupata malalamiko ya mhanga kuingiliwa kingono na babake (mrufani).

Taarifa ya kuwepo kwa tukio hilo inaanza na Gladness Amulike (SM1). Huyu ni Afisa Ustawi wa Jamii wa Halmashari ya Wilaya Iringa anayeshughulikia dawati la wenye mahitaji maalumu wakiwemo watoto. Tarehe 17/4/2023, alifika kwenye Shule ya Msingi Ulata kutoa elimu kuhusu usalama wa watoto na unyanyasaji wa kijinsia. Baada ya kutoa elimu hiyo, kwa maelezo ya SM1, ndipo mhanga (SM2) alijitokeza na kueleza kuwa baba yake humwingilia kingono majira ya usiku na ameshafanya hivyo mara 6.

Kwamba, wakati mwingine hufanya hivyo mchana watu wanapokuwa hawapo nyumbani. Kwamba, mhanga (SM2) ameshamfahamisha mama yake juu ya tukio hilo lakini hakuchukua hatua ingawa alikuwa akimtibu majeraha ya kutoka damu ukeni. SM1 alieleza pia kwamba baada ya kuwahoji watoto wawili wa kiume na wao walikiri kulawitiwa.

G. 3553, CPL Salum ni askari polisi ambaye alikuwa na Afisa Ustawi wa Jamii kwenye Shule ya Msingi Ulata na alikuwepo mhanga alipotoa maelezo yake. Mhanga alichunguzwa na Daktari Kelvin Prosper Maro ambaye alibainisha kuwa uke wa mhanga ulikuwa na dalili za kuingiliwa kwa vile ulikuwa wazi na bikra haikuwepo.

Kwa malengo ya hukumu hii, na bila kuhitimisha hivyo, nitachukulia kuwa ni kweli mhanga alikuwa ameingiliwa kingono. Hoja ninayobakia nayo kujibu ni iwapo aliyefanya kitendo hicho ni mrufani.

Ushahidi pekee wa tukio hili ni wa mrufani. SM1 na SM3 wamejaribu kueleza tukio lilivyotendeka. Hata hivyo ushahidi wao ni wa kuambiwa na mhanga (SM2) au ndugu zake wa kiume ambao hawakuletwa mahakamani kutoa ushahidi. Kinachosikitisha maelezo mazuri ya SM1 na SM3 kuhusu tukio lilivyotendeka, muda na mahali, hayako katika ushahidi wa mhanga. Mfano, SM3 (mpelelezi) anasema aliambiwa tukio lilifanyika tarehe 15/4/2023 mchana wakati mama wa mhanga alipoenda mashine kusaga unga na ndugu wa

kiume wa mhanga walikuwa wameenda kucheza. Kwamba, mrufani alikuwa akimwingilia mhanga usiku na machana na mwaka 2022 alimuingilia mara tatu. Kwamba, mrufani alimtishia asiseme chochote! Kwamba kutokana na athari za kuingiliwa, mama wa mhanga alikuwa akimtibu mhanga kwa miti shamba.

Kama mhanga (SM2) aliweza kuyasema haya yote kwa SM3 na mengine mengi kwa SM1, inasikitisha kwamba hakuyasema mahakamani. Ushahidi wake wa msingi mahakamani uko hivi:

> *"My father was beating me and also inserting mdudu wake here (pointing finger to her vagina).*

Habari za muda wa tukio, usiku au mchana, kutishiwa na kutibiwa na mama yake kwa dawa za kienyeji hazipo. Ushahidi wa SM1 na SM2 kuhusu tukio haukubaliki chini ya kifungu cha 62 cha Sheria ya Ushahidi [Sura ya 6 T.R 2022]. Ni Ushahidi wa kuambiwa.

Mama wa mhanga alifika mahakamani kutoa ushahidi kama shahidi wa pili wa utetezi (SU2). Yeye alikana kuambiwa na mhanga kuingiliwa na babake wala kumtibu kwa dawa za kienyeji. Ushahidi huu ulipuuzwa na msomi hakimu aliyesikiliza kesi ambaye katika ukurasa wa 15 wa hukumu anadai utetezi haukutikisa ushahidi wa mashtaka bila hata kueleza ni ushahidi upi wa utetezi na kwa nini anaona ushahidi wa mashtaka haujatikiswa.

Hali hiyo ya uamuzi wa mahakama ya chini imeibua lalamiko la pili kwamba ushahidi wa upande wa utetezi haukuzingatiwa. Msomi Wakili Winfrida Mpiwa anaunga mkono hoja hii. Nami, kwa sababu hukumu inayolalamikiwa haina uchambuzi wa kina wa utetezi, nakubaliana na hoja hiyo. Msomi Hakimu Mkazi Mkuu angezingatia ushahidi wa utetezi angeona kwamba ushahidi alioutumia kumtia hatiani mrufani ulikuwa ni wa kuambiwa na ulikanushwa barabara na utetezi wa mrufani. Pia angeona kwamba, ushahidi wa mashtaka kupitia kwa mhanga haukuthibitisha kuhusu namna na muda ambao tukio lilitendeka. Haitoshi kwa mhanga kusema baba yake alimwingizia mdudu ukeni.

Aidha, katika utetezi wake mrufani alisema kwamba kama mrufani angekuwa ameingiliwa kinguvu, uke wake ungechanika na asingeweza kutembea sawasawa kwa kuzingatia umri wake. Ninakubaliana na hoja hii. Mtoto wa miaka 6 hawezi kuingiliwa kingono na mtu mzima akabakia salama. Katika ushahidi wake daktari (SM4) alisema uke haukuwa na michubuko. Nimeshindwa kumwamini mhanga kuwa aliingiliwa na mrufani asimweleze mama yake katika mazingira ambayo hakuna ushahidi kuwa kuna mgogoro wa kimahusiano katika familia husika. Kitendo cha mama wa mhanga kusimama dhidi yake kinaashiria kuwa mhanga alisema uwongo. Kwa umri

wake na kwa kuzingatia mazingira ambayo tuhuma iligunduliwa, ushahidi wake unapaswa kuchukuliwa kwa tahadhari.

Rufaa hii ina mashiko, imeshinda. Mahakama ya chini ilipotoka katika kuchambua ushahidi na kumpata mrufani na hatia. Kwa sababu hiyo hatia hiyo nimeifuta na adhabu yake nimeibatilisha. Mrufani aachiliwe huru mara moja isipokuwa kama kuna sababu nyingine, tofauti na amri ya kesi hii, ya kuendelea kumshikilia gerezani.

**I.C. MUGETA**

**JAJI**

**11/6/2024**

**Mahakama:** Hukumu hii imesomwa wakiwepo Majid Matitu, Wakili wa Serikali na mrufani.

**Isw. I.C. MUGETA**

**JAJI**

**11/6/2024**